Australian Government
Department of Home Affairs

# Taarifa kwa wenye viza ya daraja la 202

## Muhtasari

Umepewa viza ya daraja dogo la 202 (Viza Maalumu ya Kibinadamu ya Kiulimwengu).

Kwa viza hii, unaweza

- kukaa Australia muda wote
- kufanya kazi na kusoma nchini Australia
- kujiandikisha katika mpango wa afya ya umma wa Australia, Medicare
- kupendekeza wanafamilia kupata ukaaji wa kudumu
- kusafiri kwenda na kutoka Australia kwa miaka 5
- ikiwa unastahiki, kuweza kupata uraia wa Australia
- kuhudhuria masomo ya lugha ya Kiingereza bila malipo kupitia Mpango wa Kiingereza wa Wahamaji kwa Watu Wazima

Hii ni viza ya kudumu. Inakuruhusu kukaa Australia muda wote Unakuwa mkazi wa kudumu siku unapoingia Australia kwa viza hii. Kwa madhumuni ya uraia, ukaaji wako wa kudumu unaanza siku unapoingia Australia kwa viza hii.

## Kuweza Kufika Australia

Wewe na mpendekezaji wako mnaweza kuwasiliana na msimamizi wa kesi yako ya Toll ili kupanga na kuweka nafasi ya kusafiri. Gharama ya usafiri ni jukumu lako au la mpendekezaji wako.

Usaidizi wa kusafiri hadi Australia unapatikana pia kupitia Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) chini ya mpango wao wa uhamiaji wa kulipia kabla ya kusafiri. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye tovuti ya IOM https://australia.iom.int/travel-assistance-migration-australia-iom-australia.

Wewe au mpendekezaji wako munapaswa kuiambia Idara kuhusu mipangilio yenu ya kusafiri ili tuweze kuhakikisha kuwa umepokea mwaliko wa kuhudhuria mpango wa Mwelekeo wa Kitamaduni wa Australia (AUSCO) kabla ya kusafiri hadi Australia na usaidizi wa makazi utakapofika Australia.

### Kadi ya ImmiCard ya Hali ya Uhamiaji ya Australia (AMS)

Serikali ya Australia inatoa AMS ImmiCard kwa wamiliki wa daraja dogo la 202 na viza zingine za kibinadamu. Kadi ya AMS ImmiCard ni hati rasmi ya kusafiri inayotimiza vigezo vya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO). Pia ni hati ya utambulisho ambayo unaweza kutumia nchini Australia ili kuthibitisha kustahiki kwako kwa huduma za serikali na kuangalia maelezo yako ya viza.

Unaweza kutumia kadi yako ya ImmiCard kama hati yako rasmi ya kusafiri kwa safari ya njia moja hadi Australia. Ina eneo linaloweza kusomeka kwa mashine ambalo huwezesha wafanyakazi wa shirika la ndege kuangalia viza yako. Ni lazima uwasilishe kadi yako ya ImmiCard kwenye uwanja wa ndege au hutaweza kusafiri kwenda Australia. Toll itakupa kadi yako ya ImmiCard kabla ya kusafiri hadi Australia.

Ikiwa una pasipoti na ungependa kuitumia kwa safari yako ya Australia, lazima utuambie kuhusiana nayo ili tuweze kuiunganisha na viza yako. Ili kutuambia kuhusu pasipoti yako, au mabadiliko ya maelezo yako ya pasipoti, nenda kwa https://immi.homeaffairs.gov.au/change-in-situation/passport-details na uchague chaguo la 'Sasisha Maelezo - Fomu ya Wavuti'. Usipofanya hivi, huenda usiweze kusafiri hadi Australia.

Ikiwa ungependa kusafiri nje ya Australia baada ya kuwasili Australia, ni lazima uwe na pasipoti halali au hati ya kusafiria isiyo ya uraia (inapatikana kutoka Ofisi ya Pasipoti ya Australia).

Ikiwa ungependa kusafiri na kurudi Australia baada ya miaka 5 kuanzia tarehe ya kutolewa kwa viza yako, utahitaji Visa ya Kurudi kwa Mkazi isipokuwa umekuwa raia wa Australia.

## Uchunguzi wa afya wa Idara

Msimamizi wa kesi yako ya Toll atakuuliza ufanye uchunguzi wa afya yako bila malipo ndani ya saa 72 kabla ya kusafiri kwenda Australia.

Uchunguzi wako wa afya wa kusafiri kuondoka unaweza kujumuisha:

- kuangalia kwamba una afya ya kutosha kuweza kusafiri
- uchunguzi wa kimwili
- kipimo cha ujauzito
- vipimo vya magonjwa ya kuambukiza
- chanjo ikihitajika, kama vile surua, mabusha na rubela
- matibabu ya vimelea na maambukizo ikiwa inahitajika

Lazima ukubali kupata matibabu kwa hali yoyote ya afya baada ya kufika Australia.

## Mpango wa Mwelekeo wa Kitamaduni wa Australia (AUSCO).

Utaalikwa kuhudhuria vipindi vya AUSCO kabla ya kusafiri kwa ushauri kuhusu safari yako ya kwenda Australia. Katika vipindi hivi utapata muhtasari wa maisha nchini Australia ikijumuisha huduma za makazi, makazi, elimu na ajira.

Madhumuni ya Mpango wa AUSCO ni:

- kutoa taarifa sahihi juu ya taratibu za kuondoka
- kuelezea mchakato wa makazi na kutoa taarifa ya vitendo kuhusu huduma za makazi baada ya kuwasili na jinsi ya kuzifikia
- kuwasilisha picha halisi ya maisha nchini Australia
- kuhimiza mafunzo ya lugha ya Kiingereza mara baada ya kuwasili Australia
- kuwapa washiriki ujuzi wa kimsingi unaohitajika ili kufikia kujitosheleza
- kuwapa washiriki zana muhimu za kushughulikia maswala ya awali ya suluhu na hatua mbalimbali za kukabiliana na utamaduni, kijamii na kiuchumi. Hii inajumuisha taarifa kuhusu sheria na kanuni za Australia.

Mpango huu wa siku 5 ni bure na uko wazi kwa wamiliki wote wa viza vya kibinadamu walio na umri wa zaidi ya miaka 5. Imeundwa ili kukupa ufahamu wa maisha nchini Australia kabla ya kufika.

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) limepewa kandarasi ya kuwasilisha programu kwa niaba ya Idara, na watawasiliana nawe ili kukualika kuhudhuria darasa la AUSCO.